

*Baadhi ya Washirika wa Huduma ya Tujenge Nyumba ya Mungu. Kutoka kulia ni Ms. Magreth Stephano, Kushoto mwa Upendo ni Mrs. Dr. Lusekelo (Glory) na wa kwanza kutoka kushoto ni Elihudi Anthony siku ya uzinduzi, tarehe 12/03/2023.*

## MWENENDO WA WASHIRIKA WA TUJENGE NYUMBA YA MUNGU

Ninamshukuru Mungu kwa uaminifu wake wa kuinua watu ambao kwa kweli wana mzigo wa utumishi ndani yao. Wamekuwa ni watu wa kujitoa kwa jinsi isiyo ya kawaida na wenye wivu na kazi ya Bwana. Wanajitoa kwa fedha, maombi, kutia moyo, muda na mali zingine ili kufanikisha kazi ya Bwana. Viwango vyao vya kujitoa vinaongezeka siku hadi siku bila kujisikia uchovu.

Washirika hawa siyo kwamba ni matajiri kiasi kwamba wana fedha za ziada badala yake katika hali ya kutambua ukuu wa Mungu wao ndio maana wanatoa kile walichonacho kufanikisha huduma hii. Wapo ambao wameajiriwa na vyeo vyao ni vya kawaida na mishahara midogo tu na wapo ambao wanabiashara ambazo ni za kawaida lakini bado wanajitoa kwa katika hali hiyo hiyo.

Kwa jinsi ya tofauti yupo mtumishi wa Mungu ndugu *Leonard Joseph* ambaye ametoa makampuni yake kuwa sehemu ya wachangiaji wa huduma hii. Yaani yeye na familia yake katika kipato chao huchangia huduma hii, lakini pia biashara yao nayo huchangia kibinafsi na hivyo kuandikwa kwenye orodha ya wachangiaji wa huduma hii.

Moja ya makampuni yake huchangia sehemu ya kumi ya kila faida inayoingia kwenye kampuni. Kampuni nyingine pia huchangia huduma hii kama wachangiaji wengine wanavyochanga. Unaweza ukajiuliza huu ni utoaji wa jinsi gani lakini katika yote tunampa Mungu utukufu. Utoaji huu unatufundisha kuwa tukumbuke kuweka mali zetu zimtumikie